

**TAARIFA KWA UMMA**



**BODI YA BIMA YA AMANA**

**KATIKA SHAURI LA MBINGA COMMUNITY BANK PLC (ILIYO CHINI YA UFILISI)**

**MALIPO YA AMANA ZILIZOWEKEWA BIMA**

Kufuatia uamuzi wa Benki Kuu ya Tanzania kuifutia **MBINGA COMMUNITY BANK PLC** leseni ya kufanya shughuli za kibenki mnamo tarehe 12 Mei, 2017, Bodi ya Bima ya Amana, Dar es Salaam, inatangaza kuanza kwa malipo ya fidia ya bima ya amana kuanzia tarehe 24 Julai, 2017 kwa waliokuwa na amana zenye kinga ya bima ya amana katika **MBINGA COMMUNITY BANK PLC** (Iliyo Chini ya Ufilisi).

Ili kufanikisha malipo ya fidia hiyo, wenye amana wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

(a) **Mahali na Muda wa Malipo**

Malipo ya fidia ya bima ya amana kwa wenye amana zilizowekewa bima yatafanyika katika **Mbinga Community Bank PLC (Iliyo chini ya ufilisi) iliyoko Mbinga, mkoani Ruvuma**. Muda wa saa za kazi utakuwa kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 11.00 jioni katika siku za kazi na kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana kwa siku za Jumamosi.

(b) **Ukomo wa Malipo ya Fidia**

Kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 kiwango cha juu kabisa cha fidia ya bima kitakachotolewa ni hadi shilingi 1,500,000.

(c) **Madai kwa amana zinazozidi Shilingi 1,500,000**

Kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, kwa wale wenye amana zinazozidi kiwango cha juu cha fidia (Shilingi 1,500,000) malipo ya kiasi kinachozidi yatafanyika kwa mujibu wa shughuli za ufilisi.

(d) **Viambatanisho vinavyohitajika**

(i) **Fomu ya Madai** iliyojazwa vizuri pamoja na nakala yake: (Inapatikana **MBINGA COMMUNITY BANK PLC** (Iliyo chini ya ufilisi) na katika tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania: [www.bot.go.tz](http://www.bot.go.tz)

(ii) Kadi ya Utambulisho wa Mwenye Amana

(iii) Utambulisho halisi wa mwenye amana kwa kuonyesha kimojawapo kati ya; Kitambulisho cha Uraia, Hati ya Kusafiria, Leseni ya Udereva au Barua ya Utambulisho kutoka kwa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa.

(d) **Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:**

**Mkurugenzi,  
Bodi ya Bima ya Amana  
Mtaa 2 Mirambo  
S. L. P 2939**

**11884 Dar es Salaam**

**Simu: + 255 22 223 5390**

Barua pepe: [DIB-INFO@bot.go.tz](mailto:DIB-INFO@bot.go.tz)

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi, Bodi ya Bima ya Amana**

Tarehe 21 Julai, 2017